



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA UMMA

**UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI KATIKA KATA
SITA (6) ZA TANZANIA BARA**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya. 292, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Udiwani katika Kata 6 zilizopo katika Halmashauri 4 na Mikoa 4 ya Tanzania Bara.

Nafasi wazi za udiwani wa Kata zimetokana na sababu mbalimbali zikiwemo Kifo, na Kujiuzulu.

Baada ya kupokea taarifa hiyo na kwa kuzingatia matakwa na masharti ya Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa; Tume ina wajibu wa kuitisha na kuendesha Uchaguzi mdogo katika Kata zifuatazo:-

Kata zilizo wazi ni kama ifuatavyo:-

Na	MKOA	HALMASHAURI	KATA	
1.	KAGERA	Halmashauri ya Wilaya ya Muleba	1.Buhangaza	Kifo
2.	MWANZA	Halmashauri ya Wilaya ya Misungwi	2.Kanyebele	Kifo
3.	SINGIDA	Halmashauri ya Manispaa ya Singida	3.Mitunduruni	Kifo
4.	KILIMANJARO	Halmashauri ya Wilaya ya Siha	4.Kashashi 5.Gararagua 6. Donyomuruak	Kujizulu Kujizulu Kujizulu

Hivyo, ninapenda kutumia nafasi hii kutoa taarifa kwa umma kuwa Tume imepanga kuendesha Uchaguzi mdogo wa Udiwani katika Kata hizo tarehe 17 Februari 2018, kwa kuzingatia ratiba ifuatayo:-

Ratiba ya Uchaguzi mdogo huo ni kama ifuatavyo:-

NA.	TUKIO	TAREHE
1.	Kutoa fomu za Uteuzi	18 – 24 Januari, 2018
2.	Uteuzi wa Wagombea Udiwani	24 Januari, 2018
3.	Kampeni za Uchaguzi	25 Januari, 2018 hadi 16 Februari, 2018
4.	Siku ya Kupiga kura	17 Februari, 2018

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inavialika Vyama vya Siasa, Wadau wa Uchaguzi na Wananchi kwa ujumla kushiriki katika Uchaguzi huo.

Mwisho, Tume inatumia fursa hii, kuviasa Vyama vya Siasa na Wadau wa Uchaguzi kuzingatia matakwa ya Katiba, Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Sura ya 292, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Madiwani) za mwaka 2015, Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2015 pamoja na maelekezo yote yaliyotolewa au yatakayotolewa na Tume katika kipindi chote cha Uchaguzi huo mdogo.

Imetolewa leo tarehe 10 Oktoba, 2017.

Jaji (R) Semistocles S. Kaijage

MWENYEKITI

TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI